# BIBLIA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  BIBLIA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

BIBLIA.

1.Biblia ni nini?…………………………………………………..

2. Jinsi kusoma biblia…………………………………………..

3. Kuokoka…………………………………………………………….

4. Mitume………………………………………………………….

5. Baraka……………………………………………………………..

6. Uponyaji…………………………………………………………..

7. Utajiri……………………………………………………………….

8.Ufalme wa Mungu……………………………………………

9.Kuomba…………………………………………………………….

10.Nabii……………………………………………………………….

11.Mchungaji……………………………………………………….

12.Mwinjilisti…………………………………………………….

13.Mhubiri…………………………………………………………..

14.Hekima…………………………………………………………….

15.Roho mtakatifu………………………………………………

16.Kuokoka…………………………………………………………

16. Mwisho………………………………………………………….

# 1. BIBLIA NI NINI?

**Biblia** ni ramani ya msafiri ya mtu aliyeokoka anasafiri kwenda makao ya mbinguni kwa wokovu yaani maisha ya mtu aliyeokoka. Anatakiwa aishi vipi ndani ya ufalme wa mungu? Awe na nini au amiliki nini? Afanye kazi ipi? Biblia ina majibu ya mafundisho au maagizo au maneno ya mungu na Yesu ya kukufikisha kwenye kila jema lilioamriwa na mungu kuja kwako au kiu yako ya haki yaani mema moyo wako una shauku nayo.

Biblia ina sehemu kuu mbili :=>

**1) Agano jipya**

Agano jipya linazunguzia Bwana Yesu na Mtu aliyeokoka (wakiwa zaidi ya mmoja na kukusanyika wanaitwa kanisa). Vitabu vya Injili (Mathayo,Yohana,Marko,Luka) vinazungumzia habari za Yesu na kidogo kuhusu kuokoka na kuanzia kitabu cha Matendo ya mitume hadi Ufunuo wa Yohana vinazungumzia ukweli wa mtu aliyeoka ukisoma kama umeokoka chagua mema.

**2)Agano la Kale.:** Agano la kale vitabu vinavyozumzia Mungu yaani Baba yake Yesu na Taifa la Mungu la Israeli wakati vitabu vya Agano jipya vinazungumzia Yesu na Kanisa mungu yu ndani ya Yesu. Yesu ni kama mungu alivyo ktk agano la kale na Kanisa ni kama Taifa la Mungu la Israeli ktk Agano la kale. Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka unapaswa kusoma biblia kila siku na kuitafakari hata saa moja mshirikishe Roho mtakatifu u mgeni ktk wokovu ndio kwanza unaanza safari ili upate kuwa Amani,Furaha na Upendo wa Mungu..

# 2. JINSI YA KUSOMA BIBLIA

Jinsi ya kusoma biblia ukaielewa sawa na mapenzi ya Mungu. Kwanza mkumbuke msaidizi wako ee mtu wa kimataifa uliyeokoka . Msaidizi huyo ni Roho mtakatifu moja usaidizi ambao yesu alisema angetupa sisi tumwaminio kama na Mwokozi ni kufundisha yote yatokayo kwa Yesu.

Kabla ya kusoma na kutafakari maandiko yaliyomo ktk biblia mwombe roho mtakatifu akufundishe yatokayo kwa Yesu . Ila ukimpenda Yesu yaani kushika neno la Yesu na kulitenda mwombe roho mtakatifu akufundishe mambo aliyokuandalia. Na pengine jinsi au njia ya kuyapata.

Jinsi ya kusoma biblia kwa kukufaidia jiuleze moyo wa unahitaji nini au haja gani? Moyo wako una kiu ipi ya haki au njaa ipi ya haki? Mfano Niombe nini yaliyo mapenzi? Utasoma maandiko yote yenye neno **omba** ktk biblia na kutafakari utafahamu ombeni nini mbele za Mungu.

Unahitaji **Mungu**. Utasoma na kutafakari maandiko yenye neno Mungu ktk biblia ukielewa ndipo utamtafuta Mungu nawe utampata ukimtafuta kwa bidii ahadi yeye kasema anapatikana.

Unahitaji **mke** . Utasoma na kutafakari maandiko yenye neno mke ktk biblia ukielewa ndipo umwombe Mungu mke.

Unahitaji **Pesa .**Utasoma na kutafakari maandiko yenye neno Pesa ktk Biblia. ukielewa ndipo umwombe Mungu akupe sawa ulivyoelewa na utende kile ulichoelewa

Unahitaji **Fedha .**Utasoma na kutafakari maandiko yenye neno Fedha ktk Biblia. ukielewa ndipo umwombe Mungu akupe sawa ulivyoelewa na utende kile ulichoelewa

Hiyo ni mifano ya haja ya moyo wako ee mtu wa kimaitaifa uliyeokoka ukiwa na masikio ya kusikia na usikie.

# 3. KUOKOKA

Kuokoka ni kuokolewa kutoka ktk maisha ya dhambi na kupewa maisha ya haki ya Yesu kama mtume Paulo ktk biblia kutoka kushika torati na kuwatesa watakatifu waliomwamini Yesu hadi kuwa na maisha ya haki kama Yesu.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno KUOKOKA utapitia mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (kuokoka) na kuitafakari ili upate mema yaliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Ukitaka maarifa juu neno KUOKOKA utatafuta vitabu ya vya watumishi vinavyozungumzia juu ya kuokoka na kuvisoma kisha kuvitafakari kwa kufundishwa na roho mtakatifu.

Mfano wa mistari ktk biblia ni ile **Marko 16 : 15 –17,Luka 21 : 36 & Rum 10:9**

**Marko 16 : 15 –17**

“Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

**Luka 21 : 36**

“Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate **kuokoka** katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.”

**Rum 10:9**

“Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, **utaokoka. “**

# 4. MITUME

Mtume ni mtumshi wa Yesu mwenye huduma ya kanisa ya  kitume. Mitume hupewa huduma na yesu kwa kusudi la kuanzisha kanisa ili awapate yesu walio wake ktk shamba(dunia) la Baba yake yaani Mungu  liliomea ngano(wateule yaani waliokoka) na Magugu (wabaya).

.Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno MTUME au MITUME utapitia mistari iliyomo ktk biblia ktk Agano jipya na kitabu cha Matendo ya mitume yenye neno hilo (Mtume au mitume ) na kuitafakari ili upate uzima/mema yaliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe . Mistari hiyo ni nuru kwa mwenye huduma ya kitume ndani yake inamfanya afahamu yaliyo mapenzi ya mungu.

Ukitaka maarifa(kujua) juu neno MTUME au MITUME utatafuta vitabu ya vya watumishi vinavyozungumzia juu ya MTUME au MITUME   na kuvisoma kisha kuvitafakari kwa kufundishwa na roho mtakatifu.

Yesu alituma mitume kuhubiri,kufundisha waliokoka ufahamu wa cheo cha Kristo(rabi) ili wayatendee ya Yesu na kuanzisha kanisa. (Mtume Petro).

**Marko 16: 14 –20** "….Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe……………………Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo……"

**Mathayo 28.19 –20**  " Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

# 5. BARAKA

Baraka ni **maongezeko** kwa kutamkiwa neno na Mungu, Yesu na Roho mtakatifu . Mungu huweza kuwatumia Mzazi aliyeokoka kwa mwanawe, mtu aliyeokoka kwa kanisa au watu au mtumishi wa Yesu.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno BARAKA utapitia mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Baraka) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno BARAKA ktk biblia soma :

**MWANZO 2 : 1 – 3**

"**Bwana** akamwambia **Abramu,** Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa **taifa** kubwa, na **kukubariki,** na kulikuza jina lako; nawe uwe **baraka**; nami **nitawabariki wakubarikio**, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. "

**Mathayo 14.19 -20** "Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile **mikate mitano** na wale **samaki wawili,** akatazama juu mbinguni, **akabariki,** akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano. Wakala wote wakashiba; wakayaookota **masazo ya vipande** vya mikate, **vikapu kumi na viwili,** vimejaa. "

**Marko 10 : 14 — 16** " Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, **akawabarikia.** "

**Luka 6.28 wabarikieni** wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi.

**Rumi 12:14** "Wabarikini wanaowaudhi; barikini, wala msilaani. "

# 6. UPONYAJI

Uponyaji ni kupona ugonjwa na mungu au Yesu kwa samehewa dhambi au uovu na Mungu ,Yesu  au Roho mtakatifu. Yesu aliwaponya watu kwa kuwawekea mikono au kuwamkia neno la uponyaji. Ziko njia kadhaa anazotumia Mungu yaani Baba yake Yesu kuwaponya wagonjwa kwa kutumia watumishi wa Yesu aliowatuma kwa kanisa.

1) Kutamka neno la uponyaji
2) Kuweka mikono juu mgonjwa
3) Mafuta ya mzeituni yaliyombewa
4) Nguo mfano leso za watumishi wa yesu kama mtume Paulo baada ya kuhudumia kanisa unachukua na kuiweka juu ya wagonjwa aliye mbali hakufika kanisani.
5) Kivuli cha watumishi wa Yesu kama mtume Petro ukimwamwangukia mgonjwa kanisani anapona au mikutano ya injili.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno UPONYAJI utapitia mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Uponyaji) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno UPONYA ktk biblia soma :

**Math.4:23 ,24 ; Math . 8: 16-17; Math. 9:22; Math.21:14 Marko 6:5**

“Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na **kuponya ugonjwa** na udhaifu wa kila namna katika watu…”

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka kama una masikio ya kusikia usikie na macho ya kuona na uone.

# 7. UTAJIRI

Utajiri au ukwasi ni kuwa na mali nyingi mfano nyumba, viwanja, mashamba,Fedha au Pesa, gari,kampuni,hoteli, viwanda, kondoo,ng'ombe,shule au chuo ktk nchi mbalimbali n.k

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno UTAJIRI utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Utajiri) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno UTAJIRI ktk biblia soma :

**Rumi 10:12** "Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye yule ni Bwana wa wote, mwenye **utajiri** kwa wote wamwitao; "

**Rumi 11:12** "Basi, ikiwa kosa lao limekuwa **utajiri** wa ulimwengu, na upungufu wao umekuwa **utajiri** wa Mataifa, je! Si zaidi sana utimilifu wao? "

**Rumi 11: 33** "Jinsi zilivyo kuu **utajiri** na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! "

**2 kor 8** "...maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na **umaskini** wao uliokuwa mwingi uliwaongezea **utajiri** wa ukarimu wao... "

**Efeso 3 : 8** " Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa **utajiri** wake Kristo usiopimika; "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka umayaelewa mambo hayo ili usi mgeni wa kusoma ramani ya kwenda makao ya mbinguni yaani Biblia yenye faida ktk wokovu (maisha mapya ndani ya Yesu) wako

# 8. UFALME WA MUNGU

Ufame wa Mungu ni utawala wa Mungu yaani Baba yake Yesu naye ni mfalme juu ya huo ufalme. Upo juu Kuliko utawala wowote au enzi au mamlaka.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno UFALME WA MUNGU utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Ufalme wa Mungu) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno UFALME WA MUNGU ktk biblia soma :

**Mathayo 21.31 ,43**

"Je! Katika hao wawili ni yupi aliyefanya mapenzi ya babaye? Wakamwambia, Ni yule wa pili. Basi Yesu akawaambia, Amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika **ufalme wa Mungu.** "

"Kwa sababu hiyo nawaambia, **Ufalme wa Mungu** utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. "

**Marko 1:15** "akisema, Wakati umetimia, na **ufalme wa Mungu** umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili. "

**Marko 4:11**

**"**Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya **ufalme wa Mungu,** bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano"

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 9. KUOMBA

Kuomba ni kupeleka haja za moyo wako mbele za Mungu yaani Baba yake Yesu. Yale unayoitaji na una uwezo wa kuyapata ktk upeo wa mawazo unaona hayawezekani kuwa nayo kwa wakati huo.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno KUOMBA utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Utajiri) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno OMBA ktk biblia soma :

**Marko 6.46** “Hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani ku**omba.** “

**Marko 11.24** “Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myao**mba**yo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. “

**Luka 6.12** “Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumw**omba** Mungu. “

**Yohana 14: 13 –14,16**

“Nanyi mki**omba** lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya. … Nami nitamw**omba** Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; “

**Yob. 16:23 – 24** “ Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimw**omba** Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; **ombeni,** nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu. “

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

## 10.NABII

Nabii ni mwonaji anayeoneshwa mambo ya baadaye na Mungu yaani Baba yake Yesu au yale mungu anayotaka kuyatenda au atakayoyatenda na kutoa unabii kwa kanisa ya waliokoka.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno NABII utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Nabii) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno NABII ktk biblia soma :

**Mathayo 2.17—18,23**

"Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na **nabii** Yeremia, akisema, Sauti ilisikiwa Rama, Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako. akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na **manabii,** Ataitwa Mnazorayo. "

**Mathayo 3 : 3**

"Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na **nabii** Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake."

**Mathayo 5:17** "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. "

**Mathayo 7:12** "Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na ma**nabii. "**

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 11.MCHUNGAJI

Mchungaji ni mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya kanisa ya kuchunga kanisa yaani waliokoka wakusanyikapo kwa jina la Yesu.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno MCHUNGAJI utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (MCHUNGAJI) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno MCHUNGAJI ktk biblia soma :

**Mathayo: 9.36**

"Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na **mchungaji.** "

**Yohana 10 : 11,12,14,16**

" Mimi ndimi **mchungaji** mwema. **Mchungaji** mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. "

"Mtu wa mshahara, wala si **mchungaji,** ambaye kondoo si mali yake, humwona mbwa-mwitu anakuja, akawaacha kondoo na kukimbia; na mbwa-mwitu huwakamata na kuwatawanya. "

"....Mimi ndimi **mchungaji** mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi; "

"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na **mchungaji** mmoja. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 12. MWINJILISTI

Mwinjilisti ni mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya kanisa ya kutangaza injili kwa kanisa.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno MWINJILISTI utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (MWINJILISTI) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno MWINJILISTI ktk biblia soma :

**Waefeso 4:11**

" Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa **wainjilisti** na wengine kuwa wachungaji na waalimu; "

Ukweli mwinjilisti wingi wake ni wainjilisti linapatikana ktk mstari mmoja tu wa biblia **Waefeso 4:11**

Na Rumi 1: 16 ni maana ya injili kama una ufahamu wa kufahamu na ni mwinjilisti ufahamu hayo. Uweza ni imani,uponyaji.miujiza.Amri ya Kutoa pepo,Ujazo wa Roho Mtakatifu ,nguvu ya utajiri,kubariki.

**Rumi 1:16**

"Kwa maana siionei haya **Injili;** kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao **wokovu,** kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 13. MHUBIRI

Mhubiri ni mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya kanisa ya

kuhubiri injili kwa wenye dhambi ili wapate kuokoka yaani kuokolewa na Maisha ya dhami na Yesu.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno MHUBIRI utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Mhubiri) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno MHUBIRI ktk biblia soma :

**Matendo ya mitume 21:8**

"Asubuhi yake tukaondoka, tukafika Kaisaria, tukaingia nyumbani mwa Filipo, **mhubiri** wa Injili, aliyekuwa mmoja wa wale saba, tukakaa kwake. "

**Rumi 10: 14**

"Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo **mhubiri**? "

**1 Timotheo 2: 7**

"Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa katika imani na kweli. "

**12 Timotheo 1: 11** 'ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe **mhubiri** na mtume na mwalimu. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

## 14. HEKIMA

Hekima ni karama apewayo mtu aliyeokoka na Mungu yaani Baba yake Yesu ni njaa ya haki ya kutafuta tafuta ufahamu na maarifa ktk mambo ya yesu na Mungu yaani Baba yake Yesu ipitayo kawaida mwanadamu ktk mambo ya Mungu

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno HEKIMA utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Hekima) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno HEKIMA ktk biblia soma :

**Mathayo 11: 18 –19**

“Maana Yohana alikuja, hali wala hanywi, wakasema, Yuna pepo. Mwana wa Adamu alikuja, akila na kunywa, wakasema, Mlafi huyu, na mlevi, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi! Na **hekima** imejulikana kuwa ina haki kwa kazi zake. “

**Mathayo 12: 42**

12.42 Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie **hekima** ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

**Matendo ya Mitume 6:3 “**Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; “

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 13. ROHO MTAKATIFU

Roho mtakatifu ni msaidizi kutoka Baba yake Yesu yaani Mungu atoaye Yesu kwa waliokoka yaani kanisa wanaomkiri Yesu ni Bwana na Mwokozi.

Ukisoma Biblia kwa kutafuta ufahamu juu ya neno ROHO MTAKATIFU utasoma mistari iliyomo ktk biblia ya kila kitabu ukianzia Agano jipya yenye neno hilo (Roho mtakatifu) na kuitafakari ili upate ufahamu uliyomo ndani ya maandiko hayo kwa kumuomba msaidizi Roho mtakatifu akufundishe.

Mfano wa maandiko ktk biblia yenye neno ROHO MTAKATIFU ktk biblia soma :

**Mathayo 1.18**

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa **Roho Mtakatifu.**

**Marko 1: 18**

“Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa **Roho Mtakatifu**. “

**Luka 1: 41** “kawa Elisabeti aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elisabeti akajazwa **Roho Mtakatifu;** “

**Yohana 14.26** “Lakini huyo Msaidizi, huyo **Roho Mtakatifu,** ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia. “

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nimeakuandikia upate ufahamu wa jinsi ya kusoma biblia ikakufaidia au kukujenga kwa kuwa unaye msaidizi wa kuthibitsha neno la kinywa Yesu kristo Yaani Roho mtakatifu aliye ndani yako.

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034